# Idhini ya Dawa za Dukani (OTC)

Sera ya Wilaya ya Shule ya Lansing po5330 inakataza wanafunzi kubeba dawa yoyote shuleni isipokuwa 'inhaler' na 'epi-pens' zilizoidhinishwa na mtoa huduma za afya.

Dawa nyingi zisizo na maelekezo ya mhudumu wa afya, za kununua dukani (OTC) kama vile dawa za maumivu, dawa za kuondoa asidi, dawa za kikohozi, losheni, mafuta ya kujikinga na miale ya jua, 'chap stick', na nyingine zinaruhusiwa shuleni kwa masharti yafuatayo:

1. Dawa ZOTE, zenye maelekezo na zisizo na maelekezo ya mtoa huduma za afya zitahifadhiwa kwa usalama shuleni kwa mujibu wa miongozo ya taratibu ya Idara ya Elimu ya Michigan. Wanafunzi **HAWATARUHUSIWA** kuwa na dawa za OTC wao wenyewe, kwenye mkoba, kwenye kabati au kwenye dawati lao.
2. Mzazi/mlezi lazima alete dawa za OTC kwenye kontena halisi kwa ofisi ya shule ili zitumiwe kwa mtoto wake.
3. Fomu ya Idhini ya Mzazi kwa Dawa za OTC Shuleni lazima ijazwe, isainiwe na kurejeshwa kwa ofisi ya shule.
4. Mzazi/mlezi anaweza kuidhinisha matumizi ya dawa za dukani, zisizo na maelekezo ya mtoa huduma za afya bila saini ya daktari.
5. Dozi na nyakati za utumiaji lazima ufanane na maelekezo kwenye kontena.

---

**Idhini ya Mzazi kwa Dawa za OTC Shuleni**

**Jina la Mwanafunzi:** **Tarehe ya kuzaliwa:**

**Jina la Dawa:**

**Dozi:** **Nyakati za utumiaji:**

**Sababu ya kutolewa:**

**Maelekezo Maalum:**

**Mzazi/Mlezi (herufi kubwa):** **Nambari ya simu:**

**Mzazi/Mlezi (saini):** **Tarehe:**